

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

Amuani ya Simu: TAMISEMI
Simu Nambari: 026-2321607,
2322853, 2322848, 2321599

Fax Namba: 026-2322116, 2321217
026-2322146, 2321013
E-mail Address: ps@pmoralg.go.tz
dlq@pmoralg.go.tz

Unapojibu tasadhali taja:

Kumb. Na. CA.26/307/01/87

Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
S.L.P. 1923,
DODOMA.



30 Oktoba, 2009

Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya,
Halmashauri za Wilaya,
TANZANIA BARA.

Wakurugenzi,
Halmashauri za Miji/Manispaa na Jiji,
TANZANIA BARA.

YAH: UKAGUZI WA MIRADI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Siku za karibuni Serikali imeendelea kupokea malalamiko mbalimbali na wakati mwingine kushuhudia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na usioridhisha. Taratibu za uendeshaaji wa Halmashauri zinaelekeza kufanyika Ukaguzi wa mara kwa mara wa miradi ili Halmashauri zihakikishe kuwepo kwa 'value for money' kwa kila matumizi yakiwemo ya miradi. Hili imebainika halitekelezwi kikamilifu kwa baadhi ya Halmashauri.

Unachukua nafasi hii kuzikumbusha Halmashauri zote nchini kwamba ukaguzi katika ngazi ya Halmashauri ni lazima kufanyika na taasisi zilizoidhinishwa kama utavyo:-

- (i) Kila Halmashauri inapaswa kuwa na Kamati ya Ukaguzi wa Miradi ambayo huongozwa na Afisa Mipango wa Wilaya. Imedhihirika Kamati hizi sehemu nyingi hazifanyi kazi, na pale zinapofanya kazi taarifa zake haziwasilishwi kunakohusika (Ofisi za Mikoa na OWM-TAMISEMI) kila robo mwaka kama inavyotakiwa.
- (ii) Vile vile Halmashauri zote zimeajiri Wakaguzi wa Ndani ambao wanatazamiwa kukagua na kuandaa taarifa za Ukaguzi kila robo mwaka. Pia Halmashauri nyingi haziwasilishi taarifa za Wakaguzi hawa kama utaratibu unavyoagiza.

- ✓(iii) Taasisi nyingine ya Ukaguzi ni Kamati ya Fedha na Uongozi/Mipango. Hii ni Kamati ya Fedha ambayo hukagua miradi kwa niaba ya Madiwani mara moja katika miez. mitatu. Pia ni sharti baada ya Ukaguzi taarifa zake zinawasilishwa kwenye vikao vya Mabaraza ya Madiwani pamoja na taarifa zingine.
- (iv) Ikumbukwe vile vile kuwa Wakuu wa Wilaya wameagiza kufanya ukaguzi wa miradi katika Wilaya zao ambao sasa inakuwa taasisi ya nne ya Ukaguzi katika ngazi za Halmashauri. Huu ndio mfumo unatarajiwa kuwepo kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Kutokana na muundo wa Ukaguzi huu na kama kila Taasisi ingefanya kazi yake ipasavyo, ni tumaini la Serikali kwamba 'value for money' ya kila Mradi itapatikana hivyo kuondoa malalmikoa ya wadau.

OWM-TAMISEMI itapenda kupata taarifa ya utekelezaji wa suala hili ikieleza kuwapo au la aina zote za Ukaguzi zilizotajwa hapo juu. Kama zipo je, zinafanya kazi yake ipasavyo?

Ofisi yangu kupitia Idara ya Serikali za Mitaa kitengo cha Ukaguzi itatembelea Halmashauri zote kujiridha utekelezaji wa maelekezo haya. Wakurugenzi wanaelekezwa kulsoma barua hii kwenye Kikao cha Kamati za Fedha inayofuatia baada ya kupokea barua hii.

Tunawatakia uzingatiaji wa suala hili kwa manufaa ya Halmashauri na Taifa kwa ujumla wake.


Kabuje, L. W.
Kny: KATIBU MKUU

Nakala: Makatibu Tawala Mikoa,
TANZANIA BARA.